# MAKAMBAKO YETU

www.makambakotc.go.tz | Kitengo cha Mawasiliano Serikalini | Halmashauri ya Mji Makambako



# ZIARA YA MADIWANI WA HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO- HALMASHAURI YA MANISPAA YA KAHAMA

**#Huduma Bora kwa Wote**

JARIDA ZIARA YA MADIWANI KAHAMA.indd 1 9/11/2023 2:24:17 PM

## UTANGULIZI

Mnamo Septemba 4,2023,Madiwani wa Halmashauri ya Mji Makambako walifanya ziara ya kutembelea Halmashauri ya Manispaa ya Kahama,Mkoa wa Shinyanga kwa lengo la kujifunza masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na Ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri,Uwekezaji na Ukuzaji wa wananchi kiuchumi.

Mara baada ya kuwasili Halmashauri ya Manispaa ya Kahama Wahe. Madiwani wakiongozana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako,Ndg. Kenneth K. Haule pamoja na baadhi ya Wakuu wa idara na Vitengo walipokelewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama,Ndg. Anderson Msumba pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri hiyo.

Katika ziara hiyo Wahe. Madiwani pamoja na Wakuu wa Idara/Vitengo walipata fursa ya kujifunza namna Halmashauri ya Manispaa ya Kahama inavyotekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati kama kuanzisha kituo cha uwezeshaji wakulima na wafugaji,eneo la uwekezaji wa viwanda la Ummy Mwalimu lenye ukubwa wa ekari 500 ,ambazo zilitolewa kwa wananchi ili kufanya uwekezaji mdogo ambapo katika eneo hilo Vijana wengi wanafanya shughuli zao katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa samani,uchomeleaji nk.

Aidha,Wahe. Madiwani wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako,Mhe. Hanana Mfikwa walipata nafasi kutembelea eneo la wafanyabiashara wadogo linalotambulika kama CDT,ambalo pia linatumika kama kituo kidogo cha mabasi,wafanyabiashara wadogo ambao walikuwa wanafanya biashara maeneo yasiyo rasmi(machinga), walipewa maeneo katika kituo hicho na kujenga vibanda na kwa sasa wanatambulika rasmi na kupata fursa mbalimbali za kujikwamua kiuchumi kama vile kupata mikopo SACCOS na kwenye taasisi zingine za kifedha.



Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako,Mhe. Hanana Mfikwa akisaini kitabu cha wageni katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama,Anderson Msumba(wa katikati),Kushoto ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako,Kenneth Haule.



Baadhi ya Wahe. Madiwani na Wakuu wa Idara/Vitengo wakimsikiliza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama walipowasili ofisini kwake.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama,Anderson Msumba akitoa taarifa ya utangulizi kwa Wahe. Madiwani wa Halmashauri ya Mji Makambako,kuhusu utendaji Kazi wa Halmashauri hiyo pamoja na mipango na Mikakati ya Halmashauri.



Mchumi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama,akitoa taarifa ya miradi na mikakati ya Halmashauri hiyo,kwa Wahe. Madiwani wa Halmashauri ya Mji Makambako kabla ya kutembelea  maeneo ya miradi.

JARIDA ZIARA YA MADIWANI KAHAMA.indd 4 9/11/2023 2:24:22 PM




Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako,Kenneth K. Haule akizungumza mara baada ya kukaribishwa katika kikao Maalumu kuhusu ziara ya Wahe. Madiwani katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.



# WAHE. MADIWANI WATEMBELEA HOSPITALI YA MANISPAA YA KAHAMA.



Wakiongozwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama,Ndg. Anderson Msumba pamoja na timu ya Menejimenti ,Wahe. Madiwani wa Halmashauri ya Mji Makambako walitembelea Hospitali ya Manispaa ya Kahama ambayo imejengwa kwa fedha za ruzuku na Mapato ya ndani.

Aidha,Wahe. Madiwani walitembelea jengo la kisasa la Uchunguzi lililopo katika Hospitali hiyo,na kujifunza namna bora ya ukusanyaji wa malipo ya huduma kupitia mfumo badala ya kupokea fedha taslimu.





# WAHE. MADIWANI WATEMBELEA ENEO LA UWEKEZAJI WA VIWANDA LA UMMY MWALIMU LA UMMY MWALIMU.



Eneo la Ummy Mwalimu la uwekezaji wa viwanda lenye ukubwa wa ekari 500,lilitengwa rasmi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda ambapo Halmashauri ilitoa maeneo bure kwa wananchi wenye uhitaji wa kufanya shughuli za viwanda ili fedha ya mtaji aliyonayo mwananchi itumike kutekeleza mradi na Halmashauri ikusanye kodi ya huduma na ushuru.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kahama,Ndg. Anderson Msumba alibainisha kuwa,ardhi hiyo ilitolewa kwa wananchi wote pamoja na vijana ambao ni wanufaika wa mikopo ya asilimia 10,inayotolewa na Halmashauri kwa vikundi vya Wanawake,Vijana na Watu wenye Ulemavu.

Msumba alisema kuwa,kwa sasa vijana ambao ni wanufaika wa mikopo ya asilimia 10,wamefanya uwekezaji wa viwanda vidogo katika eneo hilo na kukua kiuchumi kupitia viwanda vya utengenezaji wa samani mbalimbali,uchomeleaji nk.

## Baadhi ya picha katika karakana ya Richard Muhabi Mkerewe mnufaika wa mkopo wa 10%.







Wahe. Madiwani pia pamoja na wenyeji wao walipata nafasi ya kutembelea moja ya karakana ya utengenezaji wa bidhaa za aluminium kama madirisha nk na samani za ndani kama vitanda,meza,sofa,kabati nk.

Bidhaa hizo zinazalishwa na vijana kama kikundi nammoja mmoja katika eneo la Ummy Mwalimu.

Katika jengo hilo kumesheheni bidhaa zenye viwango vyenye ubo ra na ubunifu wa hali ya juu,na vijana hao kwa sasa wanapata fursa mbalimbali ikiwa pamoja na kupata mikopo nafuu kupitia benki na SACCOS.



Moja ya jengo la maonyesho (show room) ya bidhaa zinazozalishwa na Kijana Richard Muhabi Mkerewe,ambaye ni moja ya vijana ambao wlikuwa wanufaika wa mikopo ya asilimia 10,ambaye baada ya kupewa eneo na Halmashauri katika eneo la Ummy Mwalimu la uwekezaji wa Viwanda alilipia hati ya kiwanja ambayo ilimuwezesha kupata mkopo benki na kujenga karakana ya utengenezaji samani za ofisini na nyumbani.

Kwa sasa kijana huyo ana uwezo wa kuajiri hadi vijana 150.

# WAHE. MADIWANI WATEMBELEA STENDI NDOGO YA MABASI CDT INAYOTUMIKA NA WAFANYABIASHARA WADOGO (MACHINGA).



Katika eneo la stendi ndogo ya mabasi kuna zaidi ya wafanyabiashara wadogo (machinga) 400,ambao awali walikuwa wakifanya biashara maeneo yasiyo rasmi kabla ya kupewa maeneo ya kujenga vibanda katika stendi hiyo.

Wafanyabiashara hao wamejenga vibanda na wanatambuliwa na taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Halmashauri,benki na taasisi zingine za mikopo kiurahisi,hali inayowasaidia kupata mikopo inayowawezesha kufanya biashara zao na kukidhi mahitaji yao ya kila siku na kukua kiuchumi.

Kwa sasa vijana wengi ambao ni wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 waliopo kwenye eneo hilo,wana uhakika wa maisha yao kwa kupata eneo rasmi la kufanyia biashara,na kumiliki kibanda kinachomuwezesha kufanya biashara bila usumbufu na kuchangia pato la Halmashauri kwa kulipa kodi na ushuru kwa maendeleo ya Halmashauri na Taifa kwa ujumla.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Picha ya pamoja ya Wahe. Madiwani,Timu ya menejimenti ya H/Manispaa ya Kahama na H/ Mji Makambako.



# MATUKIO KATIKA PICHA



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako,Mhe. Hanana Mfikwa akitoa neno la shukurani mara baada ya kukaribishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kahama.



# MATUKIO KATIKA PICHA







# MATUKIO KATIKA PICHA





# RAMANI YA MIPAKA YA UTAWALA YA HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO




**HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO**

> **makambakotc**

> **makambakotc**

> **www.makambakotc.go.tz**

> **makambakotc**

**Jarida hili limeandaliwa na;**

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Halmashauri ya Mji Makambako**
**S.L.P 405**
**MAKAMBAKO**